

Muhtasari wa Sera na Sheria za Ardhi na Maliasili



Mwongozo kwa Lugha nyepesi wa
Sera na Sheria za Ardhi, Misititu na Wanyamapori
wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Umetayarishwa kwa
Wildlife Working Group (WWG)

Agosti 2004

Muhtasari wa Sera na Sheria za Ardhi na Maliasili

Mwongozo kwa Lugha nyepesi wa
Sera na Sheria za Ardhi, Mimitu na Wanyamapori
wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Umetayarishwa kwa
Wildlife Working Group (WWG)

Agosti 2004

Yaliyomo

| | |
|--|------------|
| Dibaji | .ii |
| Ardhi | .I |
| Sera ya Ardhi ya Taifa | .1 |
| Sheria ya Ardhi, 1999 na Sheria ya Ardhi ya Kijiji, 1999 | .2 |
| Kanuni Kuu, Wajibu na Majukumu | .2 |
| Aina za Ardhi | .4 |
| Usimamizi wa Ardhi ya Kijiji | .5 |
| Ugawaji wa Ardhi | .6 |
| Hati | .7 |
| Uhawilishaji wa Ardhi | .8 |
| Usuluhishi wa Migogoro | .9 |
| Misitu | .II |
| Maendeleo ya Jumla na Malengo ya Sera | .11 |
| Majukumu ya Jamii | .12 |
| Usimamizi wa Misitu wa Jamii kwa Ardhi ya Kijiji | .13 |
| Usimamizi wa Misitu wa Jamii kwa Ardhi ya Akiba | .15 |
| Namna jamii zinavyoweza kunufaika na Fursa Mpya katika Usimamizi wa Misitu | .16 |
| Wanyamapori | .17 |
| Usuli wa Sheria | .17 |
| Sera ya Wanyamapori Tanzania | .18 |
| Namna Sera ya Wanyamapori inavyoweza kutekelezwa | .20 |
| Ushiriki wa Jamii katika Maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori | .21 |
| Shukrani | .25 |

DIBAJI

Serikali huhitaji kuwa na mpango wa utekelezaji, unaojulikana kama Sera. Sharia husika zinatumiwa kusimamia utekelezaji wa sera na kuzisaidia kulinda ipasavyo rasilimali muhimu kama ardhi, misitu na wanyamapori. Kuna tofauti muhimu kati ya Sheria na Sera. Sera inazungumzia:

- Mipango ya Serikali kwa sekta mbalimbali, kama vile ardhi, elimu, afya, kilimo n.k.
- Namna Serikali itakavyotekeleza mipango yake
- Kuweka wazi sheria na kanuni zinazopaswa kudhibiti utoaji uamuzi

Ni Sheria na wala si Sera ambazo ndizo zinaelekeza haki muhimu, mamlaka na wajibu katika kudhibiti utekelezaji wa sera kama ya ardhi na rasilimali. Sheria zinafanua namna ya kutekeleza sera na pia:

- Kuamua ni asasi zipi na wahusika wenye haki na mamlaka ya kutoa maamuzi
- Zinaeleza adhabu inayotolewa kwa kuzivunja sheria na kanuni
- Kuzisaidia mahakama kuhimiza utekelezaji

Kwa hiyo sheria zinawaonyesha wadau mipaka na majukumu yao. Sera zinatoa mwongozo tu wa namna wadau wanavyoweza kuhusishwa.

Muhtasari huu unatoa hoja muhimu kuhusu sera na sheria zinazotawala sekta tatu muhimu za rasilimali: ardhi, misitu na wanyamapori. Taarifa iliyomo katika waraka huu imetayarishwa ili kutoa elimu kwa umma na kuvisaidia vijiji katika jamii za vijijini. Sekta za ardhi, misitu na wanyamapori zimechaguliwa kwa sababu:

Wadau ni kina nani?

Wale wote wanaoshiriki katika sera wakiwemo wale:

- wanaoathiriwa na Sera
- wanaotekeleza sera
- wanaotoa fedha za kusaidia sera.

- Umuhimu wa elimu kwa umma
- Sera na sheria zinazohusiana nazo zimepitia mabadiliko mengi hivi karibuni
- Rasilimali za sekta hizi huwapa wanavijiji njia zao za kuendeshea maisha
- Ni muhimu kwa jamii husika kusimamia ipasavyo rasilimali hizi

ARDHI

SERA YA ARDHI YA TAIFA

Sera ya kwanza ya Ardhi ya Taifa nchini Tanzania ilipitishwa mwaka 1995 kwa sababu:


- Ongezeko la idadi ya watu nchini Tanzania lilimaanisha kuwa watu wengi zaidi walikuwa wanatumia ardhi.
- Kulikuwa na migogoro mingi kati ya wakulima na wafugaji kuhusu matumizi mbalimbali ya ardhi.
- Watu wa maeneo mengi ya vijijini walijikuta hawana uhakika kuhusu haki zao za ardhi.
- Kwa kuwa baada ya uchumi kuamliwa kuwa na misingi ya soko huria suala la wawekezaji binafsi katika sekta ya ardhi ilibidi kupewa umuhimu.
- Kwa kuwa ardhi hivi sasa inaweza kununuliwa na kuuzwa kuna haja ya kudhibiti vizuri utaratibu huo.
- Kuna migogoro mingi kuhusu kutumia na kumiliki ardhi.

Changamoto!

Kwa kuwa ardhi sasa inatengwa kwa wawekezaji binafsi, je haki za ardhi za wafugaji na jamii za asili zinalindwa vipi?

Sera ya Ardhi ya Taifa inasema kuwa ardhi ya taifa imekuwa ikisimamiwa vizuri tangu tupate uhuru. Ili kutoa huduma nzuri kwa watu, inalenga:

- Kugawa ardhi bila upendeleo
- Kumpa kila mtu haki ya kutumia ardhi
- Kuhakikisha kuwa haki ya watu iliyopo kuhusu ardhi, hasa wale wasio na hati za kisheria, wanaeleweka kwa urahisi, wanakubalika na kupewa hadhi ya kisheria.
- Kuweka ukomo wa kiasi cha ardhi inayoweza kumilikiwa na mtu binafsi.
- Kuhakikisha kuwa ardhi inatumiwa kwa njia zitakazoboresha maisha ya kila mtu.
- Kuboresha na kufafanua zaidi namna ardhi hiyo inavyosimamiwa na namna migogoro inayohusu ardhi inavyoweza kutanzuliwa.
- Kuhakikisha kuwa ardhi inasimamiwa vizuri ili isitumiwe sana na iweze kuzalisha mazao kwa muda mrefu.



Sera inasema mambo muhimu kuhusu namna ardhi inavyotakiwa kusimamiwa nchini Tanzania.

- Rais ndiye aliyepewa dhamana ya umiliki wa ardhi yote nchini Tanzania kwa niaba ya Watanzania.
- Ardhi ina thamani.
- Watu hawawezi kunyang'anywa haki zao za ardhi bila ya idhini ya kisheria na malipo ya fidia kamili, ya halali na kwa wakati.
- Mabaraza ya Vijiji yatasimamia ardhi yote ya vijiji.
- Mipango haina budi kufanywa ili kuyalinda maeneo yenye umuhimu wa pekee kama vile vyanzo vya maji, visiwa, fukwe, misitu, mito, njia za kuhamahama wanyama n.k.

SHERIA YA ARDHI, 1999 NA SHERIA YA ARDHI YA VIJJI, 1999

Sheria hizi zinawaeleza watu jinsi ya kutumia, kusimamia na kumiliki ardhi Tanzania Bara.

Kanuni Kuu, Wajibu na Majukumu

Madhumuni ya sheria hizi ni kuhakikisha kuwa mawazo ya jumla na malengo ya Sheria ya Ardhi ya Taifa yanashughulikiwa. Sheria ya Ardhi inafanua wazi kuwa ardhi yote nchini Tanzania ni ya umma na Rais ndiye mwenye dhamana kwa niaba ya raia wote. Katika Serikali Kuu Rais anatoa mamlaka kwa Waziri wa Ardhi na Kamishna wa Ardhi kuhakikisha kuwa kila kitu kinafanywa vizuri. Kamishna amepewa mamlaka makubwa ya kutoa uamuzi unaohusu usimamizi wa ardhi na sasa ndiye msimamizi mkuu wa ardhi nchini.

Usimamizi wa Ardhi – Nani anafanya Nini

| | |
|-----------------------------|--|
| Rais | Mdhamini wa ardhi yote kwa niaba ya raia wa Tanzania. Anaweza akamnyang'anya mtu haki ya kutumia ardhi. Anaweza kuchukua ardhi kwa manufaa ya umma. |
| Waziri wa Ardhi | Anamsaidia Raisi na kumsimamia Kamishina wa Ardhi kuhusu masuala ya ardhi. |
| Kamishina wa Ardhi | Mhusika mkuu wa masuala ya ardhi. Humsaidia Rais kutekeleza Sheria za Ardhi. Anaweza kuwaomba watu wengine au asasi kutekeleza baadhi ya majukumu. Anafanya uamuzi muhimu kuhusu namna ardhi inavyogawanywa. |
| Halmashauri za Wilaya | Zinasaidia kueleza asasi zinazohusika kuhusu uamuzi wa usimamizi wa ardhi. |
| Mabaraza ya Vijiji | Husimamia ardhi ya kijiji kwa niaba ya Mikutano ya Vijiji. Hutoa uamuzi kuhusu maombi ya ardhi kutoka kwa wanavijiji na wageni. Hugawa ardhi ya kijiji baada ya kuidhinishwa na Mikutano ya Kijiji. Hutoa hati kwa watu ili kuonyesha kuwa wana haki ya kuishi pale walipo. |
| Mikutano ya Vijiji | Huangalia iwapo Mabaraza ya Vijiji yanasimamia ardhi ya kijiji ipasavyo. Hukubaliana kuhusu uamuzi wa mahitaji ya maisha ya kijiji yanayotakiwa kushughulikiwa. |
| Kamati za Hukumu za Vijiji | Huweka mipaka ya ardhi. Huamua nani mmiliki wa ardhi fulani. Huamua migogoro iwapo watu wataona kuwa kumefanyika kosa. Huwajibika kwa Mabaraza ya Vijiji. |
| Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji | Huamua migogoro kuhusu masuala ya ardhi katika ardhi ya kijiji. |

Changamoto!

Wafugaji na Haki za Ardhi

Mkutano wa Asasi Zisizo za Serikali kuhusu Wafugaji (PINGOs) unasema kuwa ufugaji unatoa mchango mkubwa kwa uchumi wa Tanzania, lakini manufaa yote hayo yamepuuzwa na watunga sera. Wafugaji hawajashirikishwa ipasavyo katika kutunga sera zinazowaathiri.

Ufugaji ni uti wa mgongo wa sekta ya biashara ya mifugo, hutumia kwa faida ardhi mbaya na kavu, na huwaendeshea maisha zaidi ya watanzania 400,000. Ufugaji pia ni njia ya maisha ya kiasili ambayo ni lazima itetewe na sheria.

Jambo muhimu ni iwapo sheria na sera za sasa za ardhi zinashughulikia masuala ya wafugaji na wawindaji/wakusanyaji chakula, kama vile umaskini, kutokuwa na uhakika wa ardhi, kudhurika, migogoro na watumiaji wengine wa ardhi, uharibifu wa maliasili, na kudharau maisha ya wafugaji?


Aina za Ardhi

Ardhi yote ya Tanzania imegawika katika aina tatu:

Ardhi ya Akiba ni iliyotengwa kwa ajili ya wanyamapori, misitu, hifadhi za baharini n.k. Namna maeneo haya yanavyosimamiwa yanaelezwa katika sheria zinazolinda kila sekta (k.m. Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori, Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sheria ya Hifadhi za Bahari na maeneo Tengefu, n.k.).

Ardhi ya Kijiji inajumuisha ardhi yote iliyomo ndani ya mipaka ya vijiji vilivyosajiliwa, ambapo Mabaraza ya Kijiji na Mikutano ya Kijiji vimepewa mamlaka ya kusimamia. Sheria ya Ardhi ya Kijiji inatoa maelezo ya namna usimamizi unavyotakiwa kufanyika.

Ardhi ya Kawaida ni ardhi ambayo si ya akiba wala ya kijiji na kwa hiyo, inasimamiwa na Kamishna wa Ardhi.



AINA ZA ARDHI

Usimamizi wa Ardhi ya Kijiji

Mabaraza ya Vijiji yana jukumu la kuangalia ardhi ya kijiji kwa niaba ya Mikutano ya Vijiji. Wanakijiji wana haki inayoitwa “haki ya kimila ya umiliki” inayomaanisha kuwa kama wameishi katika ardhi hiyo kwa miaka mingi wana haki nayo. Sheria ya Ardhi ya Kijiji inawapa watu wenye haki ya kimila ya umiliki, haki ya ulinzi wa kisheria sawa na wale wenyeji inayojulikana kuwa “haki ya umiliki waliyopewa”. Watu waliopewa haki ya umiliki nao wamepewa hadhi ya kisheria.

Mabaraza ya Vijiji hayana budi kuzingatia hoja hizi muhimu kwa ajili ya usimamizi wao wa ardhi za vijiji:

- Ardhi haina budi kutumika kwa hali ambayo itadumisha maisha endelevu ya watu na matumizi ya rasilimali.
- Miti, maji na rasilimali nyingine vijijini na maeneo yanayozunguka vijiji havina budi kutunzwa ipasavyo.
- Kuna vyombo vingine vya umma vyenye mamlaka kwa ardhi ya kijiji na mazingira yake na maamuzi na amri zao vinaweza kuathiri matumizi ya ardhi ya kijiji.
- Ardhi ya kijiji imo ndani ya mamlaka ya serikali za mitaa ili mamlaka hiyo iweze kuombwa kutoa maoni yao wakati mwingine.

Sheria ya Utawala wa Kijiji na Serikali ya Mitaa ya 1982

Sheria hii inazipa serikali za kijiji mamlaka ya kisheria ya kutumia, kusimamia na kumiliki ardhi na mali nyingine. Aidha inaipa jukumu serikali ya kijiji la masuala na shughuli za vijiji. Sheria hii inazipa serikali za vijiji mamlaka makubwa ya kufanya mikataba na makampuni yanayosaidia maisha na ustawi wa wanakijiji.

Sheria ya Ardhi ya Kijiji inaelekeza Mabaraza ya Vijiji kugawa ardhi yao katika aina tatu:

Ardhi ya Jumuiya

- Ni ardhi inayotumiwa na watu wengi kijijini inayojumuisha misitu, maeneo ya malisho au maeneo mengine yenye maliasili yanayosimamiwa na vikundi vya watu
- Isigawiwe kwa mtu yeyote binafsi
- Itakayojulikana kama **ardhi za kijiji za jumuiya**

Ardhi inayokaliwa ambayo imegawiwa na inatumiwa kwa ujenzi wa nyumba, kilimo, biashara n.k. na watu binafsi au familia mojamoya.

Ardhi ya matumizi ya baadaye ambayo inatengwa kwa matumizi ya baadaye ya watu binafsi au jumuiya.

Matumizi yoyote ya sehemu ya ardhi ya kijiji ya makundi hayo huamuliwa na kuidhinishwa na Mkutano wa Kijiji.

Mabaraza ya Vijiji yanaweza kufanya **mikataba ya pamoja ya matumizi ya ardhi** na Baraza moja au zaidi katika ardhi za jirani. Iwapo yanataka kufanya hivyo, kila Baraza la Kijiji halina budi kwanza:

- Kuiarifu Halmashauri ya Wilaya mipango yao.
- Kupata idhini ya kila Mkutano wa Kijiji unaohusika.

Iwapo angalau wanakijiji **mia moja** wanaona kuwa Baraza la Kijiji chao halisimamii vizuri ardhi ya kijiji na kulingana na sheria za ardhi, hawana budi kuiarifu Halmashauri ya Wilaya ambayo itamwarifu Kamishna wa Ardhi. Anaweza kuunda tume itakayopendekeza kuwa ama Halmashauri ya Wilaya au kamishna mwenyewe atakuwa na jukumu la kusimamia ardhi ya kijiji. Aidha, mwanakijiji yeyote anaweza kulishitaki Baraza la Kijiji iwapo ataona kuwa ardhi ya kijiji inasimamiwa vibaya.



Ugawaji wa Ardhi

Mabaraza ya Vijiji yana jukumu la kugawa ardhi ya kijiji lakini hawawezi kufanya hivyo bila ya idhini ya Mikutano ya Kijiji.

Mabaraza ya vijiji yanaweza kutoa haki za kimila za kumiliki ardhi kwa wanakijiji mmojammoja, familia, asasi za kijiji au wananchi wasio wanakijiji watakaopewa **“Hati ya Kumiliki Kimila”** ili kuthibitisha kuwa wanamiliki ardhi.

Vijiji vinaweza pia kukodisha ardhi kwa mtu wa nje atakayepewa haki sawa na kijiji. Haki hizi zinajulikana kama **“haki nyambu”**.

Changamoto!

Tayari kuna sheria zinazovipa vijiji mamlaka ya kudhibiti ardhi yao na rasilimali nyingi muhimu. Tatizo ni kwamba sheria hizi hazitekelezwi na mawazo mazuri yaliyomo katika sera hayatekelezwi kwa vitendo.

Serikali itafanya nini ili kuhakikisha kuwa Sheria na Sera zilizopo zinatekelezwa na ili vijiji viweze kutekeleza haki yao ya kutumia na kudhibiti ardhi?

AINA ZA UKODISHAJI

| Daraja | Kiasi cha Ardhi | Muda | Watoa uamuzi |
|-----------|----------------------------------|--------------------|--|
| Daraja A. | Hekta 5 za ardhi | Miaka 5 au pungufu | Huamuliwa na Baraza la Kijiji |
| Daraja B. | Kuanzia hekta 6 hadi 29 za ardhi | Miaka 6 hadi 9 | Huamuliwa na Baraza la Kijiji na Mkutano wa Kijiji |
| Daraja C. | Hekta 30 au zaidi | Miaka 10 au zaidi | Huamuliwa na Baraza la Kijiji, hukubaliwa na Mkutano wa Kijiji kwa kushauriwa na Kamishna. |

Kuna aina tatu za ukodishaji zinazoweza kutumiwa na watu wa nje kulingana na kiasi cha ardhi wanachohitaji na muda wanaotaka kutumia ardhi. (Angalia jedwali la hapo juu).

Endapo vijiji vinaamua kukodisha sehemu yoyote ya ardhi yao, havina budi kwanza kuhakikisha kuwa:

- Inalingana na mipango ya namna ardhi hiyo itakavyotumiwa.
- Vijiji vinaweka ardhi ya kutosha ya akiba na matumizi ya jumuiya.
- Wanapanga namna ukodishaji huo utakavyoweza kukinufaisha kijiji.

Mabaraza ya Kijiji hayatatoa ardhi kwa wageni au makampuni ya kigeni. Itakuwa kinyume cha sheria na inaweza kuhatarisha haki za kimila za kijiji za kumiliki ardhi.

Utaratibu wote hauna budi kufanywa kwenye fomu rasmi za ardhi zitakazosambazwa kwa vijiji. Utaratibu usiotumia fomu hizi rasmi hautakuwa halali.

Sheria ya Ardhi ya Kijiji inahakikisha kuwa ardhi iliyogawiwa na Mabaraza ya Vijiji kati ya mwaka 1978 na Mei 1, 2001 inapewa hadhi ya kisheria.

Hati

Vijiji havitapewa tena “hati miliki” kwa ardhi ya vijiji. Badala yake Mabaraza ya Vijiji yatapewa **Hati za Ardhi ya Vijiji** ambazo:


- Zitakayotolewa kwa niaba ya Rais.
- Zitakayokuwa ushahidi wa haki ya kimila ya kumiliki katika eneo fulani la ardhi ya kijiji.
- Zitakayoyapa Mabaraza ya Kijiji mamlaka ya kusimamia ardhi za kijiji.
- Zitakayoonyesha mipaka ya ardhi ya kijiji iliyokubaliwa na kuwekwa katika ardhi.

Uhawilishaji wa Ardhi

Rais anaweza kuhawilisha ardhi ya kijiji kuwa ardhi ya kawaida au ya akiba ambayo haitasimamiwa tena na Baraza la Kijiji. Anaweza kuamua kufanya hivyo kwa manufaa ya umma, kwa mfano iwapo ardhi inahitajika kwa uwekezaji.

Iwapo Rais na Wizara ya Ardhi wanataka kuendelea na uhawilishaji huo wa ardhi, hatua zifuatazo hazina budi kuchukuliwa:

- Maelezo ya uhawilishaji uliopendekezwa hayana budi kuchapishwa katika Gazeti la Serikali na kupewa Baraza la Kijiji.
- Kamishna wa Ardhi hana budi kuhudhuria mkutano wa Baraza la Kijiji au Mkutano wa Kijiji kueleza sababu za kuhawilishwa ardhi hiyo na kujibu maswali mengine yoyote watakayouliza wanakijiji.
- Aina, kiasi na muda wa kulipa fidia hauna budi kukubaliwa na Baraza la Kijiji na Kamishna wa Ardhi kabla ya kuhawilishwa kwa ardhi ya kijiji.
- Iwapo Kamishna wa Ardhi na Baraza la Kijiji hawatakubaliana kuhusu kiasi cha fidia itakayolipwa, basi uhawilishaji huo utasimama mpaka Mahakama Kuu itakapotoa uamuzi kuhusu kiasi cha fidia hiyo.



Waziri anaweza kutangaza eneo lolote la ardhi ya kijiji kuwa **Ardhi ya Hatari** kama ataona ni hatari mno kuimiliki au itaweza kuharibiwa kwa kukaliwa. Ardhi hiyo ni pamoja na:

- Mabwawa ya mikoko
- Maeneo chepechepe
- Ardhi iliyotengwa kwa kutupia taka za hatari
- Ardhi iliyopo katika eneo la mita sitini la kingo za mto au ziwa
- Ardhi isiyoendelezwa kutokana na udhaifu wake
- Ardhi isiyoendelezwa kutokana na umuhimu wake kwa mazingira

Kabla Waziri hajatangaza ardhi ya hatari, hana budi:

- Kuonyesha mipaka ya eneo hilo
- Kuchapisha maelezo ya ardhi ya hatari inayopendekezwa katika Gazeti la Serikali
- Kuyaarifu mamlaka ya eneo husika
- Kuwaarifu watu wote wanaomiliki eneo hilo la hatari
- Kumwarifu Rais iwapo inakaliwa na watu wenye haki za kimila. Rais atafanya mpango wa kuwalipa fidia watu hao.

Usuluhishi wa Migogoro

Kuna ngazi tano za mahakama zilizopangwa na sheria za ardhi kusuluhisha migogoro ya ardhi. Mahakama hizo kuanzia ya chini mpaka ya juu ni:

- Baraza la Ardhi ya Kijiji
- Mabaraza ya Kata
- Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya
- Mahakama Kuu (Kitengo cha Ardhi)
- Mahakama ya Ruffa ya Tanzania

Vijiji vyote havina budi kuwa na **Baraza la Ardhi la Kijiji** litakalowasaidia watu wasiokubaliana na uamuzi utakaowanufaisha wote. Wajumbe wa Baraza:

- Watakuwa watu saba, wakiwemo angalau wanawake watatu
- Watateuliwa na Baraza la Kijiji na kuthibitishwa na Mkutano wa Kijiji
- Watatumikia kwa kipindi cha miaka mitatu

Pale ambapo mipaka ya kijiji haikuamuliwa, wanakijiji hawana budi kuanza utaratibu unaojulikana kama **hukumu**. Ina maana kuwa wanahitaji kuamua mahali patakapowekwa mipaka ya ardhi ya kijiji na kuwashirikisha wale wote ambao wameathirika.

Changamoto!

Vyombo vya kutoa uamuzi vya kijiji havina budi kupewa taarifa kuhusu haki zao na wajibu wao na sheria na sera muhimu.

Mafunzo ya kuongeza uwezo kuhusu uongozi na stadi za kutolea maamuzi yataboresha uwezo wao wa kusimamia vizuri ardhi ya kijiji.

Vijiji havina budi kuunda **Kamati za Hukumu za Vijiji** zenye Wajumbe:

- Watakoachaguliwa na Mkutano wa Kijiji
- Wasiozidi tisa, wakiwemo angalau wanawake wanne
- Watatumikia miaka mitatu
- Wataruhusiwa kutumikia kwa kipindi kimoja zaidi cha miaka mitatu iwapo watachaguliwa tena.

Kamati hii itakuwa na wajibu wa kufanya yafuatayo:

- Kuamua mipaka ya ardhi ya kijiji wakati wa kutoa hukumu
- Kutenga ardhi au alama za *haki za kutumia njia ya jumuiya*
- Kutumia sheria ya kimila ili kuchambua haki za ardhi za watu walioathiriwa wakati wa kutoa hukumu
- Kulinda maslahi ya wanawake, watoto, walemavu n.k. wakati wa kutoa hukumu

Vijiji havina budi pia kumteua **Mshauri wa Hukumu wa Kijiji** ambaye:

- Ni mtu wa kuheshimika kijijini, mtaalamu, mtumishi wa umma au afisa, au hakimu
- Atateuliwa na Baraza la Kijiji

MISITU

MAENDELEO YA JUMLA NA MALENGO YA SERA

Kuna mabadiliko mengi yanayofanywa katika sheria zinazotawala misitu ya Tanzania. Sera Mpya ya Misitu ya Taifa ilitolewa Machi 1998. Tanzania imejitahidi sana kuifanya sera hiyo ifanye kazi na hatua kubwa imefikiwa kwa njia zifuatazo:

- Zaidi ya misitu ya akiba ya vijiji 600 imeanzishwa nchini.
- Mwongozo wa usimamizi wa misitu kwa kushirikisha Jamii ulichapishwa na Wizara ya Maliasili na Utalii mwezi Aprili, 2001.
- Sheria mpya ya misitu imekamilika na kupitishwa na Bunge inayoruhusu Sera ya Misitu ya Taifa kuanza kutumika.

Changamoto!

Ili tupime mafanikio, hatuna budi kujua iwapo:

- Misitu ya akiba ya kijiji inasimamiwa kwa mafanikio
- Jamii inadhibiti misitu kwa ukamilifu.
- Hakuna migogoro yoyote.

Misitu inaweza kuwa katika ardhi ya kawaida, ya akiba au ya kijiji. Jamii itakuwa na sauti kuhusu namna misitu inavyosimamiwa, kutegemea misitu hiyo iko katika mfumo gani wa utawala. Wanavijiji wanatakiwa wazingatie mambo matatu:

- Namna sheria zinavyobadilika kwa namna mapori na misitu vinavyosimamiwa nchini Tanzania.
- Vijiji vinapata nafasi ya kuanza kutunza misitu ya akiba ya jirani pamoja na ile iliyoko kwenye ardhi yao.
- Vijiji vitapewa mamlaka zaidi ya kusimamia na kudhibiti rasilimali hizi.

Madhumuni makuu ya Sera ya Taifa ya Misitu ni:

- Kuhakikisha kwamba kunaendelea kuwepo na bidhaa za misitu kunatokana na usimamizi mzuri wa maeneo ya misitu.
- Kuajiri watu wengi na kupata fedha nyingi za kigeni kwa maendeleo zaidi ya viwanda na biashara katika bidhaa za misitu ambazo zinaweza kudumishwa bila kuathiri mazingira.
- Kuhakikisha kuwa mimea yote ya aina mbalimbali na wanyama waliyomo msituni vinahifadhiwa.
- Kulinda vyanzo vya maji katika misitu.
- Kuhakikisha kuwa udongo unaendelea kuwa na rutuba.
- Kumsaidia kila mtu anayehusika kuendeleza sekta ya misitu kwa manufaa ya Taifa kwa ujumla.



Lengo kuu la sera ni kushirikisha wananchi katika kutunza misitu. Sera inasema kuwa umiliki wa ardhi na maliasili na haki ya kuvitumia ni muhimu kwa maendeleo na utunzaji wa mazingira. Uhifadhi wa mazingira unawezekana tu iwapo watu wataweza kutimizwa mahitaji yao yote, na kudhibiti rasilimali na kumiliki ardhi. Usimamizi wa jumuiya wa ardhi za kijiji, kusimamiwa na Mabaraza ya Vijiji, kutajenga mazingira mazuri kwa kuanzisha usimamizi wa misitu wa jumuiya.

WAJIBU KWA JAMII

Mwongozo wa Usimamizi wa Misitu kwa Kushirikisha Jamii wa Wizara unafafanua majukumu matatu ya wananchi katika usimamizi wa misitu.

- Kuwa **mmiliki – msimamizi** kwa upande wa Misitu ya Akiba ya Ardhi ya Kijiji au Misitu ya Akiba ya Jamii ambayo jamii ina haki ya kusimamia.
- Kuwa **Meneja mteule** kwa Maeneo ya Usimamizi wa Misitu ya Kijiji. Iwapo jamii zinaishi karibu na Misitu wa Akiba wa Taifa, Mamlaka za Jumuiya zinaweza kupewa haki ya kusimamia sehemu, ilimradi kuwe na makubaliano kati ya kijiji na mamlaka inayosimamia hifadhi.

- Kuwa **Meneja – mwenz**a na Serikali Kuu kwa Misitu ya Akiba ya Taifa au Serikali za Mitaa kwa Misitu ya Akiba ya Mamlaka ya Jumuiya. Utaratibu huu wa usimamizi wa pamoja utatawaliwa na Mikataba ya Usimamizi wa Pamoja.

Sheria ya Misitu ya 2002

Sheria mpya ya kusimamia misitu nchini kote Tanzania bara ilipitishwa na Bunge tarehe 23 Aprili, 2002. Sheria hii inatoa fursa nyingi kwa Jamii kusimamia, kutumia na kulinda misitu inayowazunguka. Sheria inasema kuwa miongoni mwa malengo yake makuu ni kuwapa wajibu na haki ya kusimamia misitu wananchi wanaoishi ndani na kandokando ya misitu.

MISITU KATIKA ARDHI YA KIJIKI

Sheria zinasema kwamba misitu na mapori katika ardhi ya kijiji havina budi kusimamiwa na Mabaraza ya Kijiji na Mikutano ya Kijiji. Mabaraza ya Kijiji yanaweza kutenga Misitu ya Akiba ya Ardhi ya Kijiji iwapo wanataka kuhakikisha kuwa misitu na mapori katika maeneo yao yanatunzwa ipasavyo. Misitu ya Akiba ya Kijiji itasimamiwa na Serikali za Kijiji au na watu wengine watakoachaguliwa na serikali za vijiji. Misitu hii ya akiba itasimamiwa ili kuzalisha rasilimali muhimu kutoka katika misitu kwa mfano miti, mbao, dawa za mitishamba, matunda n.k. Pia ulinzi wa misitu unahitajika ili kuhakikisha kwamba mazingira yanatunzwa na kwamba misitu itaendelea kuwapo. Misitu hii ya akiba itasimamiwa kulingana na mipango ya usimamizi wa misitu.



Misitu ya Akiba ya Ardhi ya Kijiji iliyotengwa na Mabaraza ya Kijiji haina budi kusimamiwa kulingana na:

- Sera zilizoamuliwa na Mabaraza ya Kijiji.
- Sheria ndogondogo zilizotungwa na Mabaraza ya Kijiji na kupitishwa na Mikutano ya Kijiji.
- Mpango wa Usimamizi wa Misitu wa Ardhi ya Kijiji.

Lazima kuwepo na **Mpango wa Usimamizi** iwapo wanakijiji watashirikishwa katika usimamizi wa misitu. Hii ni kwa sababu ni muhimu kujua kinachotakiwa kufanyika ili hatua zinazofaa zichukuliwe. Sheria inasema kwamba mipango ya usimamizi wa msitu katika ngazi ya jamii inapaswa:

- Kufafanua aina tofauti zote za rasilimali za misitu, ikiwemo mimea na wanyama, udongo na maji na namna watu wanavyozitumia kuendeshea maisha yao au kama sehemu ya utamaduni wao.
- Kufafanua namna rasilimali zinavyotumika na anayezitumia.
- Kueleza namna wanavyotarajia kunufaika kutokana na kusimamia misitu na namna itakavyosaidia uchumi, jamii na mazingira.
- Kufafanua ardhi ndani ya msitu ambapo *maeneo ya matumizi ya wenyeji* yatatengwa na haki watakayokuwa nayo watu katika maeneo hayo.

Maeneo ya Matumizi ya Wenyeji: Ni muhimu kujenga ufahamu kuhusu maeneo mbalimbali ndani ya msitu na aina mbalimbali za matumizi ya rasilimali zinaruhusiwa.

Utayarishaji wa mipango ya usimamizi ni hatua nzuri kwa jamii kutenga Misitu ya Akiba ya Ardhi ya Kijiji kwa mujibu wa Sheria:

- Mipango ya usimamizi kwa ajili ya Misitu ya Akiba ya Kijiji haina budi kuidhinishwa na Mikutano ya Kijiji na kutolewa maoni na Halmashauri ya Wilaya.
- Vijiji vinaweza kutunga sheria ndogondogo ili kusaidia mipango yao ya usimamizi.
- Vijiji vinasimamia misitu yao ya akiba kwa kipindi cha majaribio.
- Vijiji vinaweza kuomba Msitu wa Akiba wa Ardhi ya Kijiji utangazwe kwenye Gazeti la Serikali. Ili hayo yafanyike, vijiji havina budi kuomba kwa Mkurugenzi wa Misitu.



Misitu ya Akiba ya Jamii ni aina nyingine ya misitu ya akiba inayoweza kutengwa kwenye ardhi ya vijiji na vikundi vidogo vya watu ndani ya vijiji au karibu na msitu mahususi au pori katika kijiji.

Makundi hayo:

- hayana budi kuwa ni kikundi cha watu kinachotambuliwa na Baraza la Kijiji.
- yanaweza kupewa mamlaka na Baraza la Kijiji kusimamia sehemu yao ya msitu.
- hayana budi kutayarisha mpango wa usimamizi unaoeleza waziwazi madhumuni yao, shughuli na majukumu.

USIMAMIZI WA MISITU UNAOSHIRIKISHA JAMII KATIKA ARDHI YA AKIBA

Vijiji vinaweza kuingia katika **Mikataba ya Usimamizi wa Pamoja** na Misitu ya Akiba ya Mamlaka ya Serikali au ya Jamii, na ama:

- Idara ya Misitu na Ufugaji Nyuki ya Wizara ya Maliasili na Utalii iwapo ni Misitu ya Akiba ya Taifa au
- Halmashauri za Wilaya iwapo ni Misitu ya Akiba ya Mamlaka ya Serikali za Kijamii.

Sera ya Taifa ya Misitu inatoa maelezo yafuatayo ya namna ya kusimamia madhumuni ya mikataba iliyotajwa hapo juu. Inasema kuwa Mikataba ya Usimamizi wa Pamoja itaruhusu watu wote wanaopenda usimamizi na uhifadhi wa misitu kushiriki, na kwamba mikataba hii itatoa haki na manufaa kwao. Mikataba itakuwa kati ya jumuiya za wananchi na serikali kuu, mashirika mengine ya serikali, kampuni binafsi au serikali za mitaa, kutegemea hali inayohusika.

Kwa hiyo, Mikataba ya Usimamizi wa Pamoja itaipa jamii haki zaidi ya kutumia mazao ya misitu ndani ya maeneo ya akiba na kuwashirikisha wananchi kusaidia kutunza misitu ili iendelee kuzalisha.

Pia sheria inasema kwamba maudhui ya Mikataba ya Usimamizi wa Pamoja hayana budi kujumuisha yafuatayo:

- Maelezo ya msitu wa akiba uliyomo katika mkataba.
- Maelezo ya mambo yanayoshughulikiwa na mkataba.
- Nini madhumuni ya mkataba huo.
- Usimamizi wa msitu unatarajiwa kufanya nini.
- Kanuni za msitu wa akiba ni zipi (kwa mfano, nani anaruhusiwa kuingia, nani walioteuliwa kama walezi, wajibu na mamlaka yao ni nini na kuna adhabu gani kwa kuvunja kanuni hizo).

- Watu wa upande wa tatu ni kina nani, yaani watu wenye haki ya kuingia msituni lakini si sehemu ya mkataba.
- Fedha zitakazopatikana kama matokeo ya mkataba huo zitatumika katika mambo gani.
- Jinsi migogoro itakavyosuluhishwa.

Sehemu za misitu katika Misitu ya Akiba ya Taifa au mamlaka za jamii ambapo vijiji vinapewa haki ya kusimamia misitu zinaitwa Maeneo ya Usimamizi wa Misitu ya Kijiji. Maeneo haya yanasimamiwa na Mabaraza ya Kijiji iwapo watu wanataka mamlaka ya kufanya hivyo na kuidhinishwa na Mkutano wa Kijiji.

Maeneo ya Usimamizi wa Msitu wa Kijiji yanaweza kutengwa na Mkurugenzi wa Misitu mara baada ya Mkutano wa Kijiji kupeleka maombi kwake. Vijiji vinavyosimamia maeneo haya pia vinahitaji kuwa na Kamati ya Usimamizi wa Msitu wa Kijiji.

NAMNA JUMUIYA ZA WANANCHI ZITAKAVYOTUMIA FURSA MPYA KATIKA USIMAMIZI WA MISITU

Haya ni masuala yanayotakiwa kuangaliwa ili kuzingatia haja ya usimamizi wa misitu unaowashirikisha wananchi katika eneo husika:

- Rasilimali za mapori na misitu zinatumiwaje kwa upana na jumuiya za wananchi?
- Je, namna rasilimali hizo zinavyosimamiwa kwa sasa zinamaanisha kuwa zitaendelea kupatikana miaka ijayo?
- Kama jibu ni hapana, kuna matatizo gani ya namna rasilimali hizo zinavyosimamiwa?
- Iwapo wenyeji watagundua tatizo na kujionea madhara yanayofanyika, watafanya nini ili kuiboresha hali hiyo?
- Iwapo wenyeji wangeshirikishwa zaidi katika kusimamia rasilimali, italeta mafanikio gani?

Mara maswali haya yatakapokuwa yamejibiwa na jamii kwa kuzingatia miongozo, itawasaidia kuamua iwapo watatumia Msitu wa Akiba wa Ardhi ya Kijiji, Msitu wa Akiba wa Jumuiya ndani ya Kijiji au Mkataba wa Usimamizi wa Pamoja na wasimamizi wa taifa au serikali za mitaa wa msitu wa akiba wa jirani.

WANYAMAPORI

USULI WA SHERIA

Katika kipindi cha miaka 25 iliyopita **Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya mwaka 1974** imetawala usimamizi wa Wanyamapori nchini Tanzania. Sheria hii inatawala wanyamapori na rasilimali nyingine kwa njia kuu mbili:

- Kwa kuanzisha na kusimamia maeneo yanayolindwa kama vile Hifadhi za Wanyamapori na Maeneo ya Wanyamapori Yaliyodhibitiwa.
- Kwa kuratibu matumizi na ulaji wa wanyamapori na upatikanaji bidhaa za wanyamapori.

Uwindaji wa kitalii na wakazi pamoja na shughuli za utalii ni njia kuu za kutumia wanyamapori. Shughuli hizi zinadhhibitiwa na Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori. Uwindaji unafanywa katika Hifadhi za Wanyamapori, Maeneo ya Wanyamapori Yaliyodhibitiwa na maeneo ya wazi. Idara ya Wanyamapori ya Wizara ya Maliasili na Utalii inakodisha maeneo ya uwindaji, yaani maeneo katika ardhi ya akiba au ardhi ya kijiji kwa makampuni ya kitalii na uwindaji.

Katika Hifadhi za Wanyamapori:

- Haki za Watu kuingia ni finyu.
- Watu hawawezi kukata uoto bila leseni.
- Watu hawawezi kulisha mifugo yao.
- Watu hawawezi kua wanyama bila leseni.

Katika Maeneo ya Wanyamapori Yaliyodhibitiwa:

- Uwindaji unaruhusiwa ingawa unadhhibitiwa.
- Wenyeji wanaweza kuishi na kutumia ardhi kwa kilimo na kulisha mifugo.
- Watu hawaruhusiwi kula wanyamapori bila kupata leseni.



SERA YA WANYAMAPORI YA TANZANIA

Kama ilivyo ardhi na misitu, sekta ya wanyamapori nchini Tanzania inabadilika. Mabadiliko makubwa yametokana na Sera ya Wanyamapori Tanzania, iliyotangazwa na Serikali mwaka 1998. Madhumuni Makuu ya Sera ya Taifa ya Wanyamapori ni:

- Kuhakikisha kuwa aina zote za viumbe hai zinahifadhiwa.
- Kuhakikisha kwamba wanyamapori hawatumiwi kiasi cha kuifanya idadi yao ipungue.
- Kuinua mchango unaotolewa na wanyamapori katika pato la taifa na maisha ya wananchi.
- Kuhakikisha kuwa sekta ya wanyamapori inawezesha maisha yawe mazuri zaidi kwa watu masikini wa Tanzania.
- Kuhakikisha kuwa Taifa linaendelea kumiliki wanyamapori na kusimamia kwa niaba ya wananchi.

Wanyamapori nchini Tanzania wanakabiliwa na hatari nyingi zitakazosababisha idadi yao ipungue na hata wanyama kutoweka kabisa katika baadhi ya maeneo. Sera inafafanua matatizo yanayokabili wanyamapori kama ifuatavyo:

- Wanavijiji wanataka kutumia ardhi moja na wanyamapori; kwa uchache wa ardhi, idadi ya wanyamapori inaweza kupungua.
- Ushindani wa ardhi kati ya watu na wanyamapori ina maana kuwa idadi ya wanyamapori inapungua.
- Kwa kuwa watu wengi wanataka kutumia ardhi kwa ajili ya makazi, kulima, kuchunga wanyama, kuchimba madini na kukata magogo, wanyamapori wanakosa mahali ambapo kwa kawaida wanaishi na kuzaliana.
- Kuna ongezeko kubwa la biashara haramu ya wanyamapori.
- Taifa linamiliki ardhi pamoja na wanyamapori, kwa hiyo wawekezaji binafsi hawatakiwi kuendeleza viwanda vinavyohusu wanyamapori.
- Wanakijiji wana fursa chache za kutumia wanyamapori na mara nyingi hali hii inasababisha kutokujali kwao kama wanyamapori wanahifadhiwa au hapana.

Changamoto!

Kanuni za uhifadhi wa Wanyamapori (Uwindaji wa Kitalii), 2000:

- Sheria mpya iliyoongezwa katika Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya 1974 inaeleza taratibu za ugawaji wa maeneo ya uwindaji.
- Inatamka kwamba kibali cha maandishi kutoka kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori kinatakiwa ili kufanya uwindaji wa kitalii, kuangalia wanyama, safari za kupiga picha, matembezi au aina nyingine yoyote ya safari za kitalii zinazohusu wanyamapori, ndani ya maeneo ya uwindaji au kwenye eneo lililohifadhiwa.

Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ndiyo sheria mama na inatamka kuwa Idara ya Wanyamapori inaweza tu kudhibiti ukamataji, uwindaji na upigaji picha wa kibiashara wa wanyamapori. Iwapo ni kweli, ina maana kuwa serikali za vijiji zinadhibiti shughuli nyingine zote za kitalii katika ardhi ya kijiji.



Sera inatamka kuwa sekta ya wanyamapori inakabiliwa na changamoto zifuatazo katika kuhifadhi wanyamapori nchini:

- Kuwashirikisha wananchi katika kuhifadhi wanyamapori.
- Kupata fedha za kigeni nyingi zaidi.
- Kuhakikisha kuwa kuhifadhi wanyamapori na kuendeleza jamii za vijijini vinakwenda pamoja.
- Kuhakikisha kuwa rasilimali za wanyamapori zinatumiwa kisheria kwa hali itakayohakikishia kudumu kwake.
- Kuhakikisha kuwa kutunza wanyamapori ni muhimu kama ilivyo kwa matumizi mengine ya ardhi kwa wanavijiji.

Changamoto!

Nini maana ya Uhifadhi?

Uhifadhi maana yake ni kutunza miti, mimea na wanyamapori ili vyote viendelee kuwapo daima. Ina maana kutunza vyanzo vya maji ili vibaki kuwa safi na bila kufujwa. Uhifadhi maana yake hatuwezi kutumia miti mingi au kuua wanyama wengi. Iwapo tutatumia miti, lazima tupande mingine.

Zifuatazo ni baadhi ya njia za kukabiliana na changamoto hizo, kwa mujibu wa Sera ya Wanyamapori:

- Kuwashirikisha watu wengi zaidi katika kuhifadhi wanyamapori, hasa watu kutoka vijijini na sekta binafsi
- Kuhimiza wananchi kutenga Maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori ili kulinda na kuhifadhi wanyamapori nje ya Hifadhi za Taifa na Hifadhi za Wanyama.

- Kutoa haki zaidi ya mtumiaji kwa watu wanaoathiriwa na wanyamapori.
- Kufafanua wazi kwa wananchi maana ya sera ya wanyamapori ya Serikali.
- Kuwahimiza watu wengi zaidi katika sekta ya umma na binafsi kuwekeza katika shughuli ya wanyamapori.
- Kutoa sheria na kanuni zenye kusaidia ili jamii za vijijini na sekta binafsi ziweze kushirikiana kuhifadhi wanyamapori.

Sera inatamka wazi kuhusu jumuiya za kijamii: *“Ni lengo la Sera hii kuziruhusu jumuiya za vijijini na wamiliki ardhi binafsi kusimamia wanyamapori katika ardhi yao kwa manufaa yao.”*

Changamoto!

Nani anayedhibiti uwindaji wa Kitalii?


Uwindaji wa kitalii kwenye ardhi ya kijiji hivi sasa unadhibitiwa na Idara ya Wanyamapori. Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya 1974 inasema kuwa hakuna anayeruhusiwa kuwinda au kukamata wanyama katika ardhi binafsi bila leseni kutoka kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori na *kibali cha mmiliki wa ardhi*. Ardhi ya kijiji ni ardhi binafsi, kwa hiyo, mtu yeyote anayepewa leseni ya kuwinda katika maeneo haya hana budi pia kupata kibali cha Baraza la Kijiji (mamlaka ya ardhi). Mara nyingi, makampuni ya uwindaji yanaingia katika ardhi ya kijiji bila kibali cha serikali za kijiji, ambayo ni marufuku kwa mujibu wa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori.

Tabia hizi huinyima jumuiya haki ya kudhibiti ardhi yao. *Je sera iliyopo inaitaka Idara ya Wanyamapori kukubaliana na Serikali za Vijiji kabla ya kutoa leseni za uwindaji?*

NAMNA SERA YA WANYAMAPORI INAVYOWEZA KUTEKELEZWA KWA VITENDO:

- Kuendelea kuwasaidia watu wanaoathirika katika usimamizi wa ardhi na wanyamapori kuwasiliana.
- Kuanzisha njia kwa jumuiya kunufaika kutokana na wanyamapori ili wanakijiji kushiriki katika uhifadhi wa wanyamapori.
- Kukabidhi majukumu zaidi kwa vijiji na sekta binafsi kwa usimamizi wa wanyamapori katika ardhi ya kijiji.

Kwa mujibu wa Sera, kutoa haki ya mtumiaji wa wanyamapori kwa jumuiya za vijijini ili ziweze kusimamia wanyamapori itamaanisha kuwa kuwalinda wanyamapori itaonekana kuwa ni aina muhimu ya matumizi ya ardhi. Kuwapa watu kazi ya kutekeleza sera kwa vitendo kutasaidia *“kuunga mkono juhudi za serikali katika uhifadhi na usimamizi wa rasilimali za wanyamapori.”* Aidha kwa mujibu wa Sera, wananchi wanaoishi karibu na Maeneo Yaliyolindwa au maeneo yenye wanyamapori wengi wana jukumu katika kusimamia na kunufaika na wanyamapori kwenye ardhi yao wenyewe kwa kutenga Maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori.



MAENEO YA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI

Sera ya Wanyamapori inasema kuwa ni muhimu sana kuwashirikisha wananchi katika kulinda wanyamapori wa taifa. Watapewa jukumu kubwa la kusimamia rasilimali katika ardhi yao pamoja na kunufaika kutokana na wanyamapori. Njia ya kuleta mabadiliko haya itakuwa kutenga Maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori katika ardhi ya kijiji.

Sera inasema kuwa Maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori yatatengwa na serikali za vijiji ili:

- Kuhifadhi na kusimamia wanyamapori.
- Kuwapa wananchi jukumu la kutekeleza hayo.
- Kuwawezesha wananchi kunufaika kutokana na rasilimali za wanyamapori.
- Kuruhusu jumuiya kunufaika kutokana na wanyamapori kama wanavyonufaika kutokana na matumizi mengine ya ardhi yao.
- Kunufaisha wananchi kifedha ili waone thamani ya kuhifadhi wanyamapori

Serikali imetunga kanuni mpya – ili kufanikisha utelekezaji wa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya mwaka 1974 – kuhusu kutenga Maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori. Kanuni hizi ni Kanuni za Maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori za 2002.

Sheria hii mpya inaeleza namna vijiji vinavyoweza kufuata utaratibu wa kutenga Maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori katika ardhi yao. Jamii ina haki na majukumu gani katika Maeneo mapya ya Usimamizi wa Wanyamapori?:

- Vijiji vinaweza kutenga sehemu ya ardhi yao ya kijiji kwa uhifadhi. Matumizi mengine ya ardhi yanaweza kutokea katika Maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori, lakini madhumuni makuu ya maeneo haya yatakuwa kwa kuhifadha wanyamapori.
- Maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori yatasimamiwa na **Mashirika ya Kijamii** yanayowakilisha vijiji vinavyohusika na si Mabaraza ya Vijiji au Kamati za Maliasili za Kijiji.
- Mashirika ya Kijamii yatawomba Mkurugenzi wa Wanyamapori kuhalalisha kisheria Maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori (kutangaza katika Gazeti la Serikali Maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori) ili vijiji vinavyohusika viweze kupata haki za mtumiaji katika mapato ya mwaka ya wanyamapori. Mashirika ya Jamii yatathibitisha kuwa yanaweza kusimamia ipasavyo rasilimali za wanyamapori za ndani.
- Mara baada ya Mashirika ya Kijamii kupata haki za mtumiaji yatakuwa **Washiriki Walioidhinishwa** kama ilivyotamkwa katika Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori. Ina maana kwamba shirika limeidhinishwa na Mkurugenzi wa Wanyamapori kusimamia na kutumia wanyamapori katika Maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori.
- Mashirika ya Kijamii/Washiriki Walioidhinishwa watakuwa na wajibu wa kisheria wa kusimamia wanyamapori ndani ya Maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori, kwa mujibu wa mkataba wanaoufanya na Mkurugenzi wa Wanyamapori.

Namna ya Kutenga Maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori:

Kwanza Mikutano ya Kijiji haina budi kuamua kuwa wangependa kutenga Maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori kwa kutumia sehemu za ardhi ya kijiji. Kisha wawakilishi kutoka kijiji au vijiji wataunda Shirika la Kijamii. Shirika hili litasajiliwa Wizara ya Mambo ya Ndani kwa mujibu wa Sheria ya Vyama ya 1994, na halina budi kuwa na katiba halali, wanachama, sheria za maadili n.k.

Kisha wanakijiji lazima:

- Watayarishe mipango ya matumizi ya ardhi kwa kuwashirikisha wanakijiji katika mchakato wa upangaji.
- Kutenga *maeneo ya matumizi ya rasilimali* na eneo litakalojumuishwa katika Maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori.
- Wawe tayari kwa mipango yao kupitiwa ili kuona namna inavyoathiri mazingira (Tathmini ya Athari ya Mazingira).

Maeneo ya Matumizi ya Rasilimali:

Maeneo ambayo rasilimali maalum zinatumika katika sehemu tofauti za ardhi ya kijiji kutokana na mpango rahisi uliofanywa na wanakijiji.


Vijiji kupitia kwa Shirika lao la Kijamii, havina budi kutayarisha **Mpango wa Kimkakati** kwa ajili ya Maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori, wakionyesha dira yao, dhamira, mipango ya kazi n.k. Kwa maneno mengine, hawana budi kusema namna watakavyosimamia Maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori kwa manufaa ya wanavijiji.



Shirika la Kijamii/Vijiji havina budi kutayarisha **Mpango wa Jumla wa Usimamizi** wakieleza namna watakavyosimamia rasilimali, rasilimali gani zitatumika katika maeneo tofauti n.k. Hata hivyo, Kanuni za Maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori zinatamka kuwa mpango wa eneo la matumizi ya rasilimali unaweza kutumiwa mpaka miaka mitano badala ya kutayarisha Mpango wa Jumla wa Usimamizi haraka.

Mara hatua hizi zinapokamilika, Shirika la Kijamii linaweza kuomba Idara ya Wanyamapori ilipatie haki za mtumiaji kwa ajili ya wanyamapori katika Maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori yanayotarajiwa na hivyo kuwa Mshiriki Aliyeidhinishwa. Baada ya haki ya mtumiaji kutolewa Maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori yatatambuliwa rasmi. Wakati Shirika la Kijamii linapewa haki ya mtumiaji kwa wanyamapori katika Maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori, linakuwa mshiriki aliyeidhinishwa. Maana yake ni kuwa limeidhinishwa na Idara ya Wanyamapori kusimamia na kutumia baadhi ya wanyama katika Maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori.

Mara baada ya Maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori kuundwa rasmi kisheria kwa kufuata taratibu hizi, mshiriki aliyeidhinishwa anaweza kutafuta wawekezaji katika Maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori. Wawekezaji hawa wanaweza kuwa kwa ajili ya uwindaji wa kitalii, utalii wa upigaji picha au uwindaji wa mkazi. Iwapo mshiriki aliyeidhinishwa anataka mwekezaji wa utalii wa uwindaji, amwombe Mkurugenzi wa Wanyamapori kutenga eneo la utalii wa uwindaji katika Maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori. Kisha Mkurugenzi wa Wanyamapori atatoa eneo hilo kwa kampuni ya uwindaji atakayochagua mshiriki, na mshiriki aliyeidhinishwa ataingia katika mkataba na kampuni hiyo. Utalii wa upigaji picha hauhitaji kutengewa eneo lolote la uwindaji, lakini uwekezaji wote wa utalii katika Maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori nao lazima uidhinishwe na Mkurugenzi wa Wanyamapori.




SHUKRANI

Mwongozo huu katika lugha nyepesi wa Sheria na Sera za Ardhi, Misitua na Wanyamapori za Tanzania ulitengezwa kupitia msaada wa ukarimu wa mashirika ya African Initiatives, CRT Ujamaa na Sand County Foundation Community Based Conservation Network. Shukrani za kipekee ziende katika shirika la Hakikazi Catalyst kwa kuwezesha utengenezaji wa mwongozo huu; Francis Stolla wa Legal and Human Rights Centre (LHRC) kwa msaada wa kitaalam; na Nathan Mpangala kwa kuchora vikaragosi.

Imepigwa chapa na:

Colour Print (T) Limited



Kwa taarifa zaidi, wasiliana na:

Hakikazi Catalyst
Ghorofa ya 2, Jengo la Meru Plaza
Barabara ya Esso
SLP 781
Arusha
Simu/fax: 027-2509860
Barua pepe: hakikazi@cybernet.co.tz
Tovuti: www.hakikazi.org